# HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA

E- mail: uchilese27@gmail.com

Mob: +255 (0) 755311154
RUKWA- SUMBAWANGA
S . L .P 582,
KUMB.NA.USS/JOINING/F.V/07.
JULY.2022

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI UCHILE WILAYA YA SUMBAWANGA MKOA WA RUKWA 2022.

Ninafurahi kukuarifu…………………………………………………………………kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano kwa**Tahasusi ya HGK/CBG** katika shule ya sekondari Uchile mwaka**2022**. Shule hii ipo katika mji mdogo wa **Laela** umbali wa kilometa 93 kutoka Sumbawanga Mjini kufuata barabara yakwenda Mbeya, Upo usafiri wa mabasi kila siku.Kama umetokea Sumbawanga mjini Unaweza kupanda magari yaendayo Mbeya na kushuka Laela au panda magari yanayoishia Laela. Aidha kama unatokea Mbeya kwenda Sumbawanga shuka Laela, shule ipo upande wa mashariki kutoka stendi ya mabasi Laela.Unaweza kupanda bodaboda au bajaji hadi shuleni.

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe na muda utakaotangazwa na serikali bila kukosa,kuanzia saa **2 :00** Asubuhi.Mwanafunzi atakaechelewa kuripoti hatapokelewa shuleni na atakuwa amepoteza nafasi yake.

## 1:0 MAAGIZO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 1.1 SARE YA SHULE.

- Sketi Mbili(2) ziwe ndefu zenye rangi ya **NEV BLUE (1) na UGOLO (1)** (Vitamba vyote vinapatikana Laela) ili kuepuka utofauti wa rangi za vitambaa.
- Mashati mawili meupe ya mikono mirefu yenye urefu wa kutosha kuchomekea.
- Viatu jozi mbili rangi nyeusi vya kamba na visigino vifupi
- Soksi nyeupe zaidi ya pea mbili (2)
- Tai mbili (2).Moja rangi ya **UGOLO** na nyingine **NEV BLUE**
- Sweta rangi ya kijani kibichi
- T-shirt nyeusi yenye kora nyeupe
- Raba pamoja na trucksuitrangi ya **LIGHT BLUE** kwa ajili ya michezo.
- Gauni ya kitambaa cha draft ya **bluu na nyeupe**(shamba dress)

MUHIMU:
Kwa waislamu njoo na hijab yenye rangi nyeupe itakayovaliwa sambamba na sare ya shule. Aidha sarezote zitakaguliwa mara baada ya mwanafunzi kufika shuleni


Edit with WPS Office

2. ADA NA MICHANGO YA SHULE

Ada ya shule ni Tsh 70,000/=kwa mwaka,unaweza kulipa kwa awamu mbili yaani 35,000/=kwa kila muhula.

Michango muhimu inayotakiwa kwa kila mzazi/mlezi ni kama ifuatavyo;

- Tahadhari Tsh 10,000/= (hairudishwi)
- Kitambulisho Tsh 6,000/=
- Nembo ya shuleTsh2,000/=
- Taaluma Tsh 20,000/=kwa mwaka
- Ukarabati Tsh20,000/=kwa mwaka
- Mchango wa mpishi ,mlinzi,na wafanyakazi wengineTsh 30,000/=kwa mwaka
- Huduma ya kwanza Tsh 10,000/=kwa mwaka
- Mtihani wa pamoja (joint examinations) Tsh 20,000/=kwa mwaka (inatolewa mhula wa pili)

NB:Michango yote ilipwe kupitia akaunti za shule Benki ya NMB kwenye akaunti namba zifuatazo;

| AINA YA MCHANGO | NAMBA YA AKAUNTI | JINA LA BENKI | JINA LA AKAUNTI |
|---|---|---|---|
| Ada yaShule | 62101100106 | NMB | Uchile secondary school,Revenue collection account |
| Michango mingine yote | 62110007595 | NMB | Uchile secondary School,E.K account |

C. MAHITAJI MUHIMU AMBAYO KILA MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

I. Godoro la ft mbili na nusu (2.5)
II. Aje na madaftari makubwa ya kutosha kulingana na masomo yake
III. Disecting kit,na gloves pea mbili(2) (kwa wanafunzi wa CBG)
IV. Scientific calculator (kwa wanafunzi wa CBG)
V. Shuka mbili za rangi ya bluu na blanketi moja kwa ajiri ya kujikinga na baridi.
VI. Chandarua kwa ajili ya kujikinga na mbu.
VII. Kijiko,Kikombe,Sahani na Bakuri kwa ajili ya chakula
VIII. Aje na vifaa vya usafi wake binafsi kama Ndoo, mswaki n.k
IX. Ream ya karatasi 1 (A4)kwa mwaka
X. Aje na fedha ya kujikimu ya kutosha kwa ajili ya mwanafunzi mwenyewe
XI. Jalada (Spring fail) 1
XII. Picha za passport mbili (2) zenye background ya bluu akiwa amevaa sare ya shule (Shati Nyeupe)
XIII. Kila mwanafunzi aje na vifaa vya usafi yaani Jembe lenye mpini, Fyekeo, Fagio(chelewa), ndoo yenye ujazo wa lita 20,Mopa,drier na ndoo yake
XIV. Aje na kivuli Cha Cheti Cha Matokeo ya Mtihani wa Kidato Cha Nne(Result slip).


Edit with WPS Office

MUHIMU KWA WANAFUNZI WOTE:
(a)Kila mwanafunzi anapokuja kuripoti ni lazima aje na Result slip original na nakala yake moja (1)
(b)Mwanafunzi haruhusiwi kuja na mavazi ya kiraia isipokuwa aje na vitenge au kanga mbili (2)tu

3:0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.
3:1.Shule ya Sekondari Uchile inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya fuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli utakazopewa ndani na nje ya shule
- Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Evining Preparation)
- Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

*3:2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule.*

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, n.k
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendera yaTaifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba/kuwa mjamzito
10. Kugoma, kuchochea au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
11. Kukataa adhabu kwa makusudi
12. Mwanafunzi kumiliki simu ya mkononi au laini yasimu
13. Uzururaji
14. Utoro
15. Kulala nje ya shule kwa wale wanaokaa /kuishi shuleni.

*"KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI UCHILE*

-----------------------------

Neusta Nyandwi
Mkuu wa Shule.

0755311154


Edit with WPS Office

# SHULE YA SEKONDARI UCHILE

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Mimi ……………………………………………………………………………… nimesoma kwa makini maagizo yote na ninatambua kuw akuchaguliwa kwangu kuingia shule ya Sekondari ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa wameshindwa ila kwa sababu ni chache.

Hivyo,nakubali kujiunga na shule ya Sekondari Uchile. Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za Shule. Nitajitahidi kufanya kazi/kusoma kwajuhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikia na na wenzangu kweli daima.

Nitalinda hadhii/heshima ya Shule ya Sekondari Uchile na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

Tarehe…………………………..Sahihi ya mwanafunzi…………………………………………….

Mimi Mzazi/Mlezi ……………………………………………………. Nimeshuhudia motto wangu …………………………………………. Akikubali kwa hiari kujiunga na shule ya sekondari Uchile,ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi kikamilifu katika kumlea motto wangu naamini tutakuwa tunawasiliana katika kuhakikisha mwanafunzi anafanya vizuri katika masomo yake.

Tarehe …………………………………. Sahihi y aMzazi/Mlezi ………………………………………


Edit with WPS Office

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

UCHILE HIGH SCHOOL
P.O. BOX 582
RUKWA-SUMBAWANGA.
DATE…………/……………/ 2022

To: The Medical Officer
………………………………………
………………………………………
………………………………………
………………………………………
Please examine ………………………………………………………… (Name of student) as to his fitness for pursuing further education at this school.

1. Hemoglobin ……………………………………………………………………

2. P.v Blooding …………………………………………………………………..

3. (a) Blooding …………………………………………………………………..

   (b) Hearing …………………………………………………………………….

4. Blood pressure ………………………………………………………………...

5. Stool for routine examination …………………………………………………..

6. Urine for sugar ………………………………………………………………...

7. Skin diseases …………………………………………………………………..

8. Leprosy …………………………………………………………………………

9. Pulmonary tuberculosis ………………………………………………………

10. Asthma ………………………………………………………………………….

11. Epilepsy ………………………………………………………………………..

12. Deformity ………………………………………………………………………

13. Mental problem ……………………………………………………………….

14. Comment………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………..

DESIGNATION…………………………………………………………………......................


Edit with WPS Office